**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI**

SHULE YA SEKONDARI MKINDI,
S.L.P 18,
**SONGE-KILINDI.**
04/04/2022

**NAMBA ZA SIMU**
Mkuu Wa Shule
0623326866/0713281261/0755487448
Makamu Mkuu wa Shule 0655329798,0620108276
Email: mkindisecondary@gmail.com

**Kumb. Na. MKSS/E10/Vol1/01**

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

.....................................................................

S.L.P.............................................................

.......................................................................

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKINDI KIDATO CHA V-2022

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (5) katika shule ya Sekondari Mkindi mwaka 2021 tahasusi ya HGK. Shule ya Sekondari Mkindi ipo Mkoa wa Tanga Wilaya ya Kilindi umbali wa KM 25 kutoka Mji wa Handeni na Km 105 kutoka Makao makuu ya Wilaya ya Kilindi.

Ukitaka kufika Mkindi Sekondari kutokea nje ya Mji wa Handeni panda mabasi yaendayo Handeni Mjini shuka stendi kuu ya Mabasi Handeni (Chogo) kisha panda gari ziendazo Kwediboma, Songe au Kilindi kwa nauli ya Tsh 3000/= shuka kituo cha Mafleta, ukishuka hapo utapata usafiri wa pikipiki utakao kupeleka moja kwa moja shuleni Mkindi Sekondari kwa gharama ya Tsh 4000 tu. Kwa wanaoingia kwa barabara kuu itokayo Wilayani Kilindi washuke kituo cha Mafleta kisha wapande pikipiki itakayowaleta mpaka shuleni Mkindi Sekondari kwa nauli ya Tsh 4000/= tu.

Kwa watakaokuja kwa pikipiki kutokea Handeni Mjini mpaka shuleni Mkindi Sekondari wataletwa kwa nauli ya Tsh 8000/= tu.

Pamoja na barua hii naambatanisha fomu za maagizo maalumu form hizo ni:-

1. Fomu ya kukubali nafasi ya kidato cha tano (5) shule ya Sekondari Mkindi.
2. Fomu ya kupima Afya yako (iwe na muhuri wa Mganga Mkuu wa Mkoa, Wilaya , Kituo cha Afya)
3. Fomu ya mahitaji ya shule.

Kumbuka fomu namba 1 na 2 ukimaliza kujaza uje nazo Shuleni siku ya kuripoti pamoja na result slip na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

**SHERIA ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:

1. Heshima na adabu kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi, Wanafunzi wengine na Jamii kwa ujumla.
2. Utii kwa Walimu, Wafanyakazi wasio Walimu na Viranja.
3. Kuwahi kufika Shuleni na kutoondoka Shuleni kabla ya Shule kufungwa.
4. Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku za Shule.
5. Kuwahi katika kila wito (utii kwa kengele).
6. Kuvaa sare ya Shule madarasani, muda wa kazi na michezo.
7. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
8. Hairuhusiwi kutembelea vilabu vya pombe,majumba ya starehe wala nyumba ya wageni.
9. Ulevi wa aina yeyote ni marufuku.
10. Ugomvi na matusi ni mwiko.
11. Wizi, kuharibu mali/ kifaa cha Shule au kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shule, milango n.k ni marufuku.
12. Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi.
13. Ni mwiko kutupa taka/ karatasi au uchafu ovyo.
14. Urafiki wa kimapenzi hauruhusiwi Shuleni.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda nyumbani kwa Wafanyakazi bila ruhusa.
17. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vyombo vya umeme Bwenini/ darasani au mahali popote ndani ya Shule.
18. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na Simu ya mkononi Shuleni, Adhabu kali itatolewa ikiwemo kulipia uharibifu wa Mfumo wa Umeme na Mzazi kumhamisha Mwanafunzi husika.

19. Kufeli au kutofanya Mtihani au kupata alama “F” kwenye Mitihani na mazoezi darasani ni kosa
lisilo vumilika.

**MIIKO MAALUMU: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

a) Kashfa ya aina yoyote kwa Taifa kama kudharau mambo ya Kitaifa (sikukuu za Kitaifa, mikutano, wimbo wa Taifa, maandamano, nk.)
b) Wizi (kuiba).
c) Kuoa au Kuolewa.
d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
e) Kutohudhuria Shule kwa muda mrefu (utoro) bila taarifa.
f) Kupigana au Kupiga.
g) Kuchochea ghasia/ kugoma au kuongoza migomo na kuvunja amani na usalama wa
shule au watu.
h) Kuvuta sigara, kunywa pombe, bangi au dawa za kulevya.
i) Kuendesha magendo au ulanguzi wa aina yoyote.
j) Kosa la jinai, kosa likithibitishwa na polisi, au mahakamani.
k) Kulala nje ya shule bila ruhusa.
l) Kugoma adhabu.
m) Kuwa na simu ya mkononi Shuleni.
n) Ubakaji.
o) Kumpa mimba msichana ndani au nje ya shule.
p) Kutoka nje ya Shule nyakati za usiku.

# MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

## SARE ZA SHULE

### WAVULANA

(i) Suruali rangi ya Blue 2 zisiwe za kubana upana wa chini usipungue nchi 15 zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh 20,000/=
(ii) Shati nyeupe 2 zenye mikono mirefu zenye nembo ya Shule.
(iii) T-Shirt za Shule 1 Tsh: 13,000/= zenye nembo ya Shule inapatikana Shuleni.
(iv) Viatu vyeusi vya kamba vya ngozi jozi 2 visiwe na visigino virefu wala shingo ndefu wala vilivyo Chongoka,soksi rangi ya dark blue jozi 2,Mkanda mweusi wenye bakozi kubwa na uwe na upana usiozidi sm 1½ vest nyeupe 2, sweta rangi ya kijivu.

### SARE ZA MICHEZO.

(i) Raba nyeupe na soksi za michezo
(ii) (ii)Track suit rangi ya green aple yenye mistari meupe zenye nembo ya adidas na nembo ya shule inzinapatikana Shuleni kwa gharama ya Tsh 25,000/=
(iii) Uje na Jezi rangi nyeusi full

### SARE ZA KUSHINDIA

(i) Suruali 2 za kaki zisiwe Modo
(ii) T-Shirts 2 rangi ya gold zenye nembo ya Shule zinapatikana Shuleni kwa Tshs 12000/= tu.

### WASICHANA

(i) Sketi 2 mshono wa V rangi BlueKitambaa Cha Lucas zinazo vuka magoti iwe pana ya kutosha na isibane kwenye hips zinapatikana Shuleni kwa gharama za Tshs. 20,000/=
(ii) Mashati meupe jozi 2 yenye mikono mirefu
(iii) Singlend nyeupe 2 za kuvaa ndani ya Shati la Shule.
(iv) Blazia zinazo ruhusiwa ni nyeupe tu.
(v) Kwa Wanafunzi wa kiislam washone Sketi mpaka kwenye usawa wa Kifundo cha mguu zisizo bana na kuonyesha hips na nusu kanzu hijabunyeupe
(vi) Viatu vya Shule vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kufunga kamba au vinavoitwa Juma na Roza.
(vii) Soksi nyeupe freesize jozi 3
(viii) Sweta la Shule rangi ya kijivu..

(ix) T-Shirt za Shule 1 yenye nembo ya Shule ,inapatikana Shuleni kwa Tshs 13,000/=

**SARE ZA MICHEZO.**

(i) Aje na Raba nyeupe na soksi za michezo
(ii) Tracksuit rangi ya green aple yenye mistari mieupe nembo ya Adidas na nembo ya shule, Zinapatikana Shuleni kwa gharama ya 25,000/= tu

**SARE ZA KUSHINDIA**

(i) Sketi 2 rangi ya kaki mshono wa solo ndefu mpaka fundo la mguu.
(ii) T-Shirts 2 rangi ya gold zenye nembo ya Shule zinapatikana Shuleni kwa Tsh 12,000/=
(iii) Mitandio 2 rangi ya creame na isiyo na urembo kwa wanafunzi wa Kiislam.

**MAHITAJI YA MALAZI KWA WOTE**

- Shuka za pink kwa wasichana na light blue kwa wavulana
- Mto 1, foronya 2, chandarua 1 cheupe kwa wasichana , na blue kwa wavulana
- Ndoo ndogo 1 na kubwa 1
- Taulo kwa wote , kanga pair 2 kwa wasichana
- Nguo za kulalia kwa wote
- Malapa ya kuogea
- Godoro futi 2 ½ upana na unene nchi 4

**VIFAA VYA USAFI**

- Ufagio 1 wa chelewa usio na mti kwa ajili ya kufagilia nje
- Ufagio wa ndani (soft broom) 1 wasichana
- Ruber squeezer 1 kwa wavulana
- brush ngumu zenye mshikio wa mti za kusugulia vyoo kwa wote
- Wavulana waje na jembe na wasichana kwanja

**MAHITAJI MENGINE YA KUJANAYO SHULENI BILA KUKOSA**

1. Sanduku la bati (Tranka) na kufuli
2. Madaftari makubwa counter book quire 3 nane na madogo 8 yanayoanzia kurasa 200 kwa ajili ya mazoezi.
3. Kalamu za kutosha
4. Mkebe wa mahesabu
5. Calculator
6. Rim 2, moja ya mistari na nyingine A4 isiyo na mistari
7. Vyombo vya chakula: sahani, bakuli, kikombe na kijiko viwe vya mfupa au vya udongo na hotpot ndogo
8. Aje na Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

9. Aje na Tsh 5000/= kwa ajili ya kitambulisho
10. Pesa ya nembo 5000/

# ADA NA MICHANGO YA SHULE

| AINA YA MICHANGO | MUHULA WA 1 | MUHULA WA 2 | JUMLA |
|---|---|---|---|
| ADA | 35,000/= | 35,000/= | 70,000/= |
| TAALUMA | 10,000/= | 10,000/= | 20,000/= |
| HUDUMA ZA AFYA | | | |
| | 10,000/= | | 10,000/= |
| TAHADHARI | 5000/= | | 5000/= |
| UPISHI | 5000 | 5000 | 10000 |
| DAWATI | 15000 | - | 15000 |
| ULINZI | 5000/= | 5000/= | 10,000/= |
| UKARABATI | 10,000/= | | 10000 |
| UMEME | 5000/= | 5000/= | 10,000/= |
| MAHAFALI | 10,000/= | | 10,000/= |
| **JUMLA** | **110000** | **60000** | **170000/=** |

***NB: MALIPO YOTE YAFANYIKE KUPITIA AKAUNTI NAMBA YA SHULE***

***AMBAYO NI 42610000565 NMB – JINA LA AKAUNTI MKINDI SECONDARY SCHOOL***

Mwanafunzi aje na nakala halisi ya Benki Slip ikiwa imeandikwa jina halisi la Mwanafunzi,hatupokei pesa cash za ada na michango Mingine.

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS

MKINDI SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 90,
**SONGE – KILINDI**

Date......................

**MEDICAL OFFICER, GOVERNMENT HOSPITAL**

.......................................................
NAME OF STUDENT...............................................
Please examine the above named student to ascertain his fitness for admission to pursue studies.

..............................................
**Head Mistress/Headmaster**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin...................................................................................................
Eyes...................................................................................................
Ears...................................................................................................C
hest...................................................................................................
Spleen...............................................................................................
Abdomen...........................................................................................
Urine...................................................................................................
Stool...................................................................................................He
moglobin(Hb).....................................................................................
I consider that:

1. He is of good health, free from infectious diseases, worms, bilharzias and fit to pursue studies
2. He is now fit to return to school after having been treated for................

...............................................................**Name and Designation**
**Signature**

**................................** **............................**
**Official StampDate**

## UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KUINGIA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MKINDI

**SEHEMU A:** (Ijazwe na Mwanafunzi)

Mimi (jina kamili)……………………………………………………………………………………

Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………………………………………

Dini……………………………………………………………………………………………………

Kijiji…………………………… Wilaya………………………… Mkoa…………………………

Nakubali nafasi niliyopewa ya kuingia Kidatocha Tano Shule ya Sekondari Mkindi. Nathibitisha kuwa Nitatii na kufuata sheria zote za Shule kama zilivyo ainishwa. Najua na kuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiriki katika Migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa uongozi wa Shule ili matatizo yatafutiwe ufumbuzi pindi yanapotokea.

Saini……………………………………..
Tarehe……………………………………

**SEHEMU B:** (Ijazwe na Mzazi)

Mimi (Jina kamili) …………………………………………Namba ya simu……………………

KIjiji……………………………  Wilaya………………………… Mkoa…………………………

Nafurahi kupokea nafasi aliyopata mwanangu Nitatekeleza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu kulingana na maagizo ya Shule. Nitahakikisha mtoto anaenda shule muda uliopangwa na nitakuwa tayari wakati wote kusaidiana na Shule kumlea mtoto huyu kinidhamu na kimaadili.

Saini ya Mzazi
……………………………………………….Tarehe……………………………………

Jina la Mtendaji wa Kijiji……………………………………………………………

Saini………………………………… Tarehe…………………………
Mhuri…………………….

Jina la Mtendaji Kata………………………………………………………………….

Saini………………………………… Tarehe…………………………

Mhuri……………………………

**ANGALIZO**

Hakikisha unafika Shuleni ndani ya wiki ya kwanza ya kufungua shule na mwisho wa kuripoti ni wiki mbili kuanzia tarehe ya kufungua Shule na baada ya hapo nafasi yako atapewa mtu mwingine endapo utakua hujafika Shuleni.

**KAULI MBIU YETU; "MKINDI BILA DARAJA LA PILI HAKIKA INAWEZEKANA"**

KARIBUNI SANA MKINDI SEKONDARI

……………………………………

**CHUKI A. ATHUMANI**

**MKUU WA SHULE**